Ser. No. EDU 220/18

# CHUO KIKUU CHA GARISSA

## MTIHANI WA MWISHO WA SEMISTA

Idara ya **Sanaa na Sayansi ya Kijamii** Shahada ya **Elimu (B.Ed-Arts)**

Semista ya **Pili 2017/2018** **KIS 220: Fasihi Simulizi katika Kiswahili**

Muda: **Saa 3** Tarehe:**11/4/2018**

Mkondo**: Regular**

**Maelekezo:** Jibu swali la **KWANZA** na maswali mengine **MATATU**
Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**

---

1. (a) Jadili kwa mifano mwafaka jinsi mbinu zifuatazo za utafiti zinavyotumiwa na watafiti wa fasihi simulizi:
   i. Mahojiano **[Alama 3]**
   ii. Hojaji **[Alama 3]**
   iii. Uchunguzi shiriki **[Alama 3]**

   (b) Eleza masuala yoyote MATANO yanayoweza kufanyiwa utafiti katika fasihi simulizi katika jamii ya kisasa. **[Alama 5]**

   (c) Jadili manufaa yoyote MATANO ynayotokana na kufanya utafiti wa nyanjani. **[Alama 5]**

   (d) Eleza changamoto zozote SITA zinazoweza kumkabili mtafiti wa fasihi simulizi anayekusanya data nyanjani. **[Alama 6]**

2. (a) Fafanua sifa zozote TANO zinazotambulisha ngomezi. **[Alama 5]**

   (b) Tathmini umuhimu wa ngomezi katika jamii ya kisasa. **[Alama 10]**

3. (a) Jadili kwa mifano mwafaka sifa zozote TANO bainifu za tendi. **[Alama 5]**

   (b) Toa maelezo mafupi yanayofafanua vipera vifuatavyo vya maghani:
   i. Sifo **[Alama 2]**
   ii. Pembezi **[Alama 2]**
   iii. Tondozi **[Alama 2]**
   iv. Rara **[Alama 2]**
   v. Majigambo **[Alama 2]**

4. (a) Fafanua changamoto zozote TANO zinazoibuka wakati wa kuainisha tanzu za fasihi simulizi ya Kiafrika. **[Alama 5]**